TANGAZO LA SERIKALI NA.154 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA CHITEMO YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Chitemo ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH1 yenye majira - nukta 189237.813MS, 9291052.428KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ35$^0$09’18.36’’MS kwa umbali wa kilomita 10.81 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH2 yenye majira - nukta 195463.067MS, 92822176.074KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS18$^0$16’21.18’’MS kwa umbali wa kilomita 4.17 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji nambaCH3 yenye majira - nukta 196772.629MS, 9278209.955KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS72$^0$54’05.79’’MG kwa umbali wa kilomita 11.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH4 yenye majira - nukta 186081.599MS, 9274921.293MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS12$^0$20’30.84’’MG kwa umbali wa kilomita 8.50 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH5 yenye majira - nukta 184262.684MS, 9283234.378KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ58$^0$58’49.02’’MG kwa umbali wa kilomita 3.54 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba CH6 yenye majira - nukta 187296.489MS, 9285058.693KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ18$^0$00’48.78’’MG kwa umbali wa kilomita 6.26 hadi ulipoanzia.”

Dodoma
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*